KANUNI YA KISASI (MALIPIZO)

Katika maisha tunafundishwa sana kuepuka kisasi (kulipiza

ubaya kwa ubaya). Nimekuwa pia nikihubiri sana kupitia

vitabu na makala mbalimbali ninazoandika kuhusu suala

la kuepuka tabia ya kulipiza kisasi kwani ni jambo baya na huharibu

maendeleo binafsi (personal development) ya mtu.

Pia kulipa kisasi huongeza chuki na migogoro katika jamii badala

ya kuunganisha jamii.

Katika kujadili mada hii ya kanuni ya kulipiza kisasi katika suala la

mahusiano, tutaongelea aina mbili za kisasi. Kisasi cha kwanza ni

kile kijulikanacho na wengi, kulipa ubaya kwa ubaya na kisasi

cha pili kinaitwa kulipa wema kwa wema.

Katika mahusiano, aina zote mbili za kisasi hufanya kazi na ni

vyema kulifahamu hili vizuri, kwani, kushindwa kulifahamu hili

matokeo yake ndiyo yale ya kulalamikia mpira unaodunda wakati

aliyeudundisha ni wewe mwenyewe.

Kama unakumbuka, mwanzoni mwa kitabu hiki nilisema, kitabu

hiki kimelenga kumsaidia msomaji kwa kuusema ukweli unaofumbiwa macho kwa kufunika kombe ili mwana haramu apite!

Hapa sitafunika kombe maana mwana huyu haramu hana mpango

wa kupita, bali ameamua kuishi miongoni mwetu na tusipokuwa

wawazi ataendelea kuishi nasi na kutuletea shida zaidi na zaidi.

Sasa, hebu tuangalia hizi aina mbili za kisasi katika mahusiano na

kwenye ndoa;

KISASI CHA WEMA KWA WEMA

Haya ni malipo yanayotokana na wema uliofanya (mshahara wa

kazi uliyoifanya). Malipo haya mara nyingi huja tu yenyewe

(automatically) ndani ya akili na hisia za mlipaji baada ya kuwa

amefanyiwa jambo jema. Malipo haya yanakuwa tofauti kidogo na

mshahara wa ofisini ambao kuna wakati mwajiriwa hupaswa kuudai

baada ya mwajiri kujisahau au kutokuwa tayari kulipa kutokana na

changamoto alizonazo.

Malipo haya katika mahusiano hupaswi hata kuyadai ukishafanya

kazi yako, tena kuna wakati yatakuwa ni surprise kwako (yanakuja

bila matarajio yako) na katika ukubwa ambao haukuutarajia. Malipo

haya huwa ni ya kihisia zaidi na siyo ya mali. Hata kama

yakiandamana na mali, lakini kiongozi wake huwa ni hisia.

Nimesema malipo haya ni mshahara. Baada ya wewe kufanya kazi

nzuri kinachofuata huwa ni haya malipo ya kihisia (mshahara wako).

Jambo baya ni kuwa, watu wengi katika mahusiano hutaka

mshahara kabla ya kufanya kazi. Watu hutaka haki kabla ya

kutimiza wajibu.

Sikia, mshahara ni matunda ya kazi, haki ni matunda ya wajibu.

Usitarajie mshahara kama hujafanya kazi na usitarajie kupata haki

kama hujatimiza wajibu. HAIKO HIVYO!

Kabla hujalalamika kuwa hakujali, jiulize wewe unamjali kwa kiasi

gani? Kabla hujalalamika kuwa siku hizi hakupendi, jiulize wewe

unamthibitishia upendo wako kwake au unasimamia kauli za

vijiweni eti ukimwonesha unampenda sana atakudharau? Sasa kama

unamchukulia poa ili asikudharau unataka akulipe nini kama siyo

kukuchukulia poa na wewe?

Kabla hujalalamika hajali kuhusu ndugu zako, jiulize, wewe baada

ya yeye kukwambia kuhusu ugonjwa wa mama yake ulichukuliaje?

Alipokuja ndugu yake kuwatembelea ulijihusisha naye kwa kiasi

gani? Au ulikuwa bize na mafaili ya kazini ndugu yake ulimkabidhi

aongee na TV? Unataka malipo mema hapa? Eti ndugu zako

wapendwe na kuthaminiwa sana na mwenza wako na asipofanya

hivyo unamlalamikia na kumuona mbaya! Hivi, hapa unashindwaje

kujua kuwa mpira unaoulalamikia kudunda kwake uliudundisha

mwenyewe?

Mwanamaarifa mmoja aliwahi kusema, "If you want her to treat

you like a King, treat her like a Queen." (Kama ukitaka mwenza

wako akutendee kama mfalme, mtendee kama malkia).
Na kama unataka akutendee na kukuchukulia kama malaika,

mtendee na umchukulie kama mfalme. Kila chema unachokitaka

kutoka kwa mwenza wako huwa ni matokeo. Hakiji tu hivi hivi, ni

matokeo ya kile chema ulichotenda wewe.

Kanuni ya kisababishi na matokeo (Law of cause and effect)

hufanya kazi vizuri pia katika mahusiano. J ifunze kuamini kuwa,

kila jambo unalolitaka kwa mwenza wako ni matokeo ya sababu

utakayoifanya ili imwezeshe kukupa matokeo hayo. Haiwezi

kutokea tu.

Inawezekana umegundua mwenza wako amekusaliti mara kadhaa,

usiwe kama watu wengi wafanyavyo, kukimbilia tu kusema

wanaume wote ni mbwa au wanawake wote 'hawajatulia,' usiwe

hivyo.

Ukijikuta katika hali hiyo, ikumbuke kanuni ya kisababishi na

matokeo (law of cause and effect). Usaliti huo ni matokeo, lazima kuna kisababishi (cause) cha matokeo hayo. Usipambane na matokeo, maana ni vigumu kupata suluhu, pambana kujua sababu ya matokeo hayo na ujikite katika kuitatua sababu siyo matokeo.

Ukiangalia sababu huenda ukagundua wewe ndiye kisababishi na ikiwa hivyo maana itakuwa ni rahisi kwako kutatua tatizo kwani suluhu yake itakuwa ni wewe kujirekebisha tu na siyo kushikana mashati na mwenza wako.

Wapo watakaosema kuwa, '**kama mtu anakupenda kwa sababu umemfanyia kitu na usipomfanyia hakupendi tena, basi huyo hakupendi achana naye.'**

Naomba unielewe vizuri, lengo la kitabu hiki ni kuvunja ukimya unaoficha ukweli unaoweza kuisaidia jamii, na nitaendelea kufanya

hivyo mpaka mwisho wa kitabu hiki.

Ipo hivi, mahusiano ni suala linaloongozwa zaidi na hisia na

kusaidiwa na kufikiri (thinking). Huenda ukanielewa kwa mfano

huu, Rais Nelson Mandela alipotoka gerezani baada ya kuwekwa

gerezani na wazungu kwa miaka 27 alitangaza msamaha kwa

wazungu waliomfunga gerezani kwa muda wote wa miaka 27.

Alitangaza hadharani kuwa aliwasamehe. Lakini, shujaa huyu wa

Afrika alishindwa kumsamehe mkewe aliyemsaliti na kutembea na

mwanaume mwingine kipindi yeye akiwa gerezani. Jaribu kujiuliza

kati ya waliomfunga Mandela kwa miaka 27 na mkewe aliyemsaliti

ni nani hasa aliyesababisha matatizo na nani kati ya wakoloni na

mkewe alistahili msamaha wa haraka?

Sitaki kuingilia maamuzi ya shujaa Nelson Mandela wala sitaki

kusema kuwa hakuwa sahihi au alikuwa sahihi. Hayo ni ya

Ngoswe, acha tumwachie Ngoswe mwenyewe.

Ninachotaka kukuonesha ni namna ambavyo mapenzi hayana

komandoo na kuwa kwa kiasi kikubwa huongozwa na hisia na siyo

uwezo mkubwa wa kufikiri.

Hebu jaribu kujiuliza juu ya mtu unayemwambia kila siku

"Nakupenda." halafu anaitikia bila kujali, "Poa". Unadhani

utakomaa mpaka lini hata kama ni kweli unampenda? Kuna wakati

tu hisia zitaanza kuchoka na utashangaa haukuwa tayari kabisa

kuruhusu aende lakini utaanza kuona basi kama hakuelewi ni sawa aende tu. Ile nguvu ya kwanza ya kusema hauko tayari kumwacha

aende imeenda wapi?

J iulize "yule mtu uliyesema mimi nampenda na nitaolewa naye

hivyo hivyo hata kama hanipendi." Na kweli ukafosi mpaka

ikawezekana, lakini baada ya kuendelea kupuuzwa ndani ya ndoa,

leo hutaki ndoa unaona huwezi kuendelea kuishi na mwanaume

asiyekupenda, umechoka! Ile nguvu uliyokuwa nayo mwanzo

iliyokufanya mpaka uingia kwenye ndoa unayojua kabisa hupendwi

imeenda wapi?

Ndugu rafiki, mahusiano hufuata kanuni ya malipizo, anaweza

akawa anakuvumilia leo akiamini kesho utabadilika na kumlipa

mshahara wa wema wake kwako. Utamlipa upendo kwa

kumrudishia upendo. Lakini usipofanya hivyo, hata kama

alikupenda vipi mwanzo kuna wakati hisia zake zitachoka na

ataanza kubadilika baada ya kuona hakuna malipo ya mema

atendayo katika mahusiano yenu. Hakuna mtu anapenda kufanya

kazi bila malipo mpendwa.

Hivyo, malipizo hayaepukiki katika mahusiano ambayo kikawaida

huongozwa na hisia. Hakikisha unatimiza wajibu wako. Timiza

wajibu wako katika mahusiano yako kutokana na jinsia yako,

mpende na ajue, mshauri, msaidie anapohitaji msaada, mlindie siri

zake, msaidie kubadilika kwenye mambo unayodhani anastahili

kubadilika, muoneshe ni wa muhimu kwako na atakufanya wa

muhimu kwake n.k.

Ukifanya kinyume na haya, tarajia matokeo ya kinyume na hayo na

hapo hutakuwa na wa kumlaumu zaidi yako mwenyewe.

KISASI CHA UBAYA KWA UBAYA

Kisasi hiki ni kile cha ubaya ambacho mara zote huwa tunaonywa

kutokukifanya. J ambo baya ni kuwa, mahusiano mengi hutembea

katika mstari wa kisasi hiki. Si vyema kabisa kuishi katika kisasi

cha aina hii lakini kwa sababu watu wengi waliopo katika ndoa

huishi katika maisha ya kisasi cha aina hii, hatuna budi

kukizungumzia bila kufumba macho.

Usimfanyie ubaya mwenza wako, kwani, kwa kiasi kikubwa ubaya

huo utalipwa wewe baada ya muda. Utavuna ulichopanda.

Ukipanda mahindi utavuna mahindi na ukipanda mpunga utavuna

mpunga. Haiwezekani kupanda mtama ukavuna mapapai. Hata

Biblia imeweka wazi kuwa, kipimo utumiacho kuwapimia wengine

ndicho hicho hicho ambacho utapimiwa wewe.

Kama hujui lipi ni jema na lipi ni baya kumtendea mwenza wako,

basi kabla hujafanya jambo jiulize hivi, "Hivi jambo kama hili

endapo mwenza wangu atanitendea mimi, nitalifurahia?

Nitajisikiaje?" Ukiona ni jambo ambalo litakukwaza kama

ukitendewa wewe basi hilo ni jambo baya achana nalo usimfanyie

mwenziyo.

Kama wewe ni mwanandoa, jiulize, hivi kama sisi wanandoa

tukifanya sote kama nachotaka kufanya mimi, hii ndoa itakuwaje?
Ukiona suala hilo litaleta furaha kwenu nyinyi nyote, basi endelea

nalo. Lakini ukiona litamkwaza mmoja wenu, tafadhali liache mara

moja kwa maana malipo ya tendo hilo yatarudi kwako baada ya

muda mfupi tu.

Njia hii ikusaidie katika maisha yako ya kila siku. Uwapo ofisini,

kabla hujaiba mali ya ofisi, jiulize, "hivi itakuwaje kama kila mtu

ofisini hapa ataamua kuiba mali za ofisini hapa kama mimi?"

Kabla hujatukana watu barabarani, jiulize, hivi itakuwaje kama kila

mtu ataamua kutukana watu barabarani kama wewe? J iulize,

itakuwaje kama kila mtu atakuwa mwaminifu kazini, kwenye ndoa

au kwa marafiki kama wewe? Kisha fuata majibu mema ya maswali

hayo. Fanya kitakachosababisha hayo matokeo mazuri yenye kuleta

maendeleo.

Ieleweke kuwa, kulipiza ubaya kwa ubaya ni adhabu kwako

mwenyewe kwa kuwa, badala ya kukupa amani huzidi kukukosesha

furaha na amani yako na ya wengine pia. Kisasi cha ubaya

huchochea tatizo na kulikuza zaidi kuliko kulimaliza.

Kwa mfano, kama utasalitiwa na wewe ukaamua kulipa kisasi kwa

kusaliti pia, hapa matokeo yake kama uliyemsaliti atagundua, hata

kama alikusaliti na yeye mwanzo, hilo haliwezi kumaliza tatizo

badala yake hali itakuwa mbaya zaidi kwani hakutakuwa na

kuaminiana tena, hakutakuwa na upendo tena na pengine hata

kuthaminiana kutapungua na kinachofuata bila shaka ni kifo cha

penzi lenu.

Hakuna aliyewahi kushinda kwa kisasi cha ubaya kwa kupata

matokeo mazuri.

Hivyo, naomba kueleweka kuwa, nimesemea juu ya kisasi cha

ubaya kwa kuwa, kuna watu wengi huishi nacho kwa kudhani kuwa

ni tiba juu ya mabaya waliyotendewa, hivyo, usimtendee mwenza

wako ubaya kwani huenda akawa ni miongoni mwa wale walipa

visasi akakulipa ubaya.

Hata kama akiwa si mlipa visasi, kumbuka Mungu katika vitabu

vya dini ameahidi kuwalipia visasi watu wema wasiotaka kulipa

visasi. Kuwa makini maana ubaya wako unaweza kukutana na

kisasi cha Mungu.

Jambo muhimu unalotakiwa kulielewa ni kuwa..... (kinaendelea)

KUKIPATA KITABU CHOTE FULL WASILIANA NASI KWA NAMBA 0769 884 844/ 0677 433 702

AU INGIA MOJA KWA MOJA kwenye mtandao wa getvalue.co utakipata hapo

Email: hojamwalimu@gmail.com

michaelmtanzania@gmail.com